

## Sina Zaidi na Hadithi Nyingine


“... Akionja tu basi, atakuwa renga karengwa, atakuwa mrija kinywani mwako ufyonze utakavyo, bila kizuizi bila kinyang'anyiro kati yako na mahasidi. Atakuwa farasi uliyemrakibu na kumshikia lijamu; popote utakapokwenda atakupeleka, lolote upendalo akutende atakutendea...”

“...anashuka... Anamsaidia Maji Marefu kulisukuma gari, huku Sam kaushika usukani na kujaribu kuliwasha. Baada ya kulisukuma sana linawaka. Maji Marefu analikimbilia, anafungua mlango na kuingia ndani... anasubiri lisimame...”

*Sina Zaidi na Hadithi Nyingine* ni mkusanyiko wa hadithi fupi wenye ubora wa namna yake. Mkusanyiko huu unajumuisha hadithi zilizoandikwa na waandishi wazoefu na wenye ustadi mkubwa katika kuogelea bahari tata ya utanzu huu wa hadithi fupi.

Waandishi hawa wamethibitisha kwa hadithi hizi umahiri wao sio tu wa kusarifu lugha ya Kiswahili vilivyo na kwa namna ya kupigiwa mfano, bali pia kwa kutawala mbinu mahsusi zinazoendana na utanzu huu. Wasomaji wa mkusanyiko huu wa hadithi fupi, wa ndani na nje ya shule na vyo vilevile, watauonea ureda uwiano bora unaoibuliwa kati ya fani na maudhui anuwai kwenye hadithi mbalimbali zilizomo humu.

Wahariri wa Mkusanyiko huu ni wasomi, watafiti, wahakiki na waandishi maarufu. Ken Walibora ni Profesa Mwandamizi katika Idara ya Fasihi na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Wisconsin, Marekani. Dkt. P. I. Iribemwangi ni Mhadhiri wa Isimu ya Kiswahili katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi.



Sina Zaidi na Hadithi Nyingine

Ken Walibora na P. I. Iribemwangi

# Sina Zaidi

na Hadithi Nyingine



Ken Walibora  
P. I. Iribemwangi  
(Wahariri)

 **Target**  
PUBLICATIONS LIMITED  
Unveiling your Potential

ISBN: 978-9966-002-77-8



9 789966 002778

